

TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM



SALAMU ZA MKUU WA TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM (DIT) PROF. PREKSEDIS MARCO NDOMBA KWA WANAJUMUIYA WA TAASISI KATIKA KUUAGA MWAKA 2016 NA KUUKARIBISHA MWAKA MPYA WA 2017

Ndugu Wanajumuiya ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema na uwezo wake ambao umetufikisha katika kipindi hiki cha kuuaga mwaka 2016 na panapo majaaliwa yake tutaingia katika mwaka mpya 2017 tukiwa wenye nguvu, afya na ari ya utendaji kazi.

Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza wote kwa ushirikiano mlionipa katika kutimiza malengo ya uwepo wa Taasisi hii ambapo kwa kipindi kifupi nilichokaa hapa tumepiga hatua kubwa katika kujenga misingi ya ufanisi kwa siku za usoni. Hata hivyo, mwaka 2016 ulikuwa wa kipekee kwani ulitawaliwa na matukio mengi yakiwemo ya furaha, huzuni na simanzi.

Ninawapongeza wale wote ambao mmepata mafanikio ya kikazi na kijamii kama vile kuhitimu masomo, kupanda vyeo, kuteuliwa katika nyazifa mbalimbali, kujenga nyumba, kuoza au kuolewa au kupata watoto ndani ya mwaka 2016.

Aidha, kwa masikitiko makubwa ninatoa pole sana kwa wale wote waliofikwa na matukio ya simanzi kwa kuondokewa na ndugu na jamaa zao wa karibu; lakini pia kwa Taasisi yetu kuondokewa na baadhi ya wafanyakazi na wanafunzi wake.

Pamoja na ukweli kwamba niliteuliwa kuiongoza Taasisi hii katikati ya mwaka yaani mnamo tarehe 10 Mei 2016 na kuanza rasmi majukumu yangu mnamo tarehe 1 Julai 2016, kwa ushirikiano wenu tumeweza kufanya mambo mengi makubwa ambayo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, mathalani;-

- i) Tumeanzisha mfumo wa uboreshaji wa utoaji mafunzo kwa wanafunzi (Teaching Material Concept);
- ii) Tumeanza mchakato wa kuboresha sheria ya uanzishwaji wa Taasisi na miongozo mbalimbali ya kiutendaji ya Taasisi;
- iii) Tumeendelea kusisitiza na kuboresha utekelezaji wa tathmini ya utendaji kazi (OPRAS) kwa kupitia semina mbalimbali;
- iv) Baraza jipya la Taasisi limeundwa na limeanza kazi rasmi;
- v) Tumefanikiwa kuzingatia ushirikishwaji wa watumishi katika ngazi zote kwa kufanya mikutano ya Baraza la Wafanyakazi na mikutano mbalimbali ya kiutawala;
- vi) Tumeendelea kuimarisha uhusiano na wadau wetu wa maendeleo kama vile Ubalozi wa Korea Kusini, Ubalozi wa India, Ubalozi wa Italia Ofisi ya Benki ya Dunia iliyopo Dar es Salaam, Umoja wa Ulaya n.k.;
- vii) Tumefanikiwa kufanya matukio ya utoaji Tuzo kwa wanafunzi na pia Mahafali ya Kumi ya Taasisi yetu kwa muda muafaka kama ilivyopendekezwa na wadau wetu;
- viii) Tumefanikiwa kuanzisha programu ya mafunzo ya Sayansi ya Maabara na Teknolojia ya muda mrefu katika Kampasi ya Mwanza.
- ix) Kwa ujumla hali ya utendaji kazi katika Taasisi yetu imeendelea kuimarika;

Kwa hayo yote na mengine ya aina hiyo ninawapongeza na kuwashukuru wanajumuiya wote kwa michango yenu ya hali na mali katika kufanikisha utekelezaji na mipango ya Taasisi.

Sasa mwaka 2016 umefikia ukingoni na mbele yetu tunauona mwaka 2017. Ni matumaini yangu kuwa Mungu atatujalia wote kufika salama mwakani.

Aidha, ni vema pia kama Taasisi kujipangia malengo tunaposubiri kuukaribisha mwaka 2017. Kwa mantiki hiyo basi hatuna budi kujiwekea malengo ya mwakani ambayo yatakuwa ndiyo dira katika mustakabali wa Taasisi yetu.

Aidha, Naomba kuchukua fursa hii kuainisha matarajio ya kimkakati ya Taasisi yetu hapo mwakani.


- i) Kuendelea Kuimarisha utoaji mafunzo ili tuweze kuzalisha wahitimu wanaoweza kujiajiri;
- ii) Kuboresha tafiti na machapisho ili kuimarisha uwezo wa wanataaluma na kutoa mchango wa kitaalam kwa jamii inayotuzunguka;

- iii) Kuongeza udahili wa wanafunzi ili kukidhi soko la ajira kwa kuzingatia azma ya Serikali yetu kuwa nchi ya viwanda;
- iv) Kumalizia mradi wa Teaching Tower Complex kwa lengo la kuboresha miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- v) Kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii;
- vi) Kuongeza na kuboresha huduma za maktaba;
- vii) Kuanzisha programu mpya ya muda mrefu ya ngozi katika Kampasi ya Mwanza;
- viii) Kuanza kutoa mafunzo ya ufundi katika Kampasi ya Myunga, mkoani Songwe; na
- ix) Mwakani tunatarajia kuadhimisha jubilee ya Taasisi ya miaka 60 tangu ilipoanzishwa mwaka 1957.

Tutaendelea kuendesha na kusimamia mikutano/makongamano mbalimbali ya kiutafiti ya ndani na nje ya nchi.

Ni matumaini yangu kuwa, tutaendelea kushirikiana sote katika kufikia malengo hayo tuliyojiwekea.

Ninawatakieni heri na fanaka tunapomaliza Mwaka 2016 na Heri ya Mwaka Mpya 2017.



Prof. Preksedis M. Ndomba

MKUU WA TAASISI